6. RATIBA YA MWAKA 2015 HUDUMA ZA UINJILISHAJI

Ratiba ifuatayo imepangwa kwa ajili ya huduma za Uinjilishaji, malezi na uponyaji:

	TUKIO	TAREHE
1	**UZINDUZI WA HUDUMA ZA UINJILISHAJI**	**31 MEI – ASKOFU MKUU**
2	Huduma za Uponyaji na Kufunguliwa	**Jumatano: Saa 4 – 6; na 11-01**
3	Huduma za Ushauri	**Alhamisi Saa 4 - 12 Jioni**
4	Semina ya Imani Katoliki	**19 – 28 Juni**
5	Semina ya Uongozi – Sehemu ya kwanza; awamu ya I	**24 – 27 Septemba**
6	Semina ya Biblia	**04 – 11 Oktoba**
7	Semina ya Ndoa	**25 Oktoba – 1 Novemba**
8	Semina ya Uongozi – Sehemu ya kwanza; awamu ya II	**26 – 29 Novemba**
9	Semina ya vyama vya kitume na mikondo ya kikatoliki	**Itapangwa na Kutangazwa**
10	Huduma ya uponyaji kwa njia ya Ekaristi Takatifu	**Itapangwa na Kutangazwa**

RAMANI YA JIMBO KUU KATOLIKI LA ARUSHA



7. MIPANGO YA BAADAYE

Mipango ya siku za karibuni ya kituo ni:

A. Kujenga ukumbi wa kudumu kwa ajili ya semina, mikutano na mahubiri.
B. Kuanzisha radio na gazeti la Jimbo Kuu la Arusha.
C. Kujenga Hosteli bora kwa ajili ya semina na malezi.



CONTACTS

Dr. Alex Lengeju +255786533776

Mr. Peter Nassary +255754207454

Mr. Apolinay P. Shiyo +255 762876338

JIMBO KUU KATOLIKI LA ARUSHA KITUO CHA MT. PAULO CHA UINJILISHAJI NA MAWASILIANO



"Ninyi ni chumvi ya Dunia...

Ninyi ni nuru ya Ulimwengu"

(Mt. 5:13-14)

1. UTANGULIZI:

Baada ya kuhitimisha maadhimisho mwaka wa Jubilei ya Jimbo Kuu Katoliki la Arusha na kwa kuitikia wito wa Baba Mtakatifu Benedikto XVI wa Kanisa la Afrika kuwa chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu (*Africa Munus)*; tunadhamiria kuifanya lengo la **Uinjilishaji wa Kina** kuwa Dhamira yetu Kuu na ya kudumu, ili Kanisa liendelee kuwa hai. Kufanikisha azma hii, tutakuwa na programu ya kulea na kuendeleza Uinjilishaji wa Kina kama zoezi la kudumu. Ili kufanikisha programu hii, tumeamua kukifanya kilichokuwa Kituo chetu cha Malezi Unga Limited kuwa **Kituo cha Mt. Paulo Mtume cha Uinjilishaji na Mawasiliano** Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.

Jina la Mt. Paulo limechaguliwa makusudi kwa sababu mbili za msingi. Moja, Mt. Paulo alikuwa Mwinjilishaji Mkuu wa Kanisa la Kwanza. Kwa njia yake, Injili ya Yesu Kristo ilienea katika dunia yote ya wakati ule. Pili, kwa njia ya Nyaraka zake, Mt. Paulo alikuwa Mwanahabari Mkuu wa Kanisa la kwanza. Ni sala yetu kwamba kituo hiki kitazawadiwa ari, nguvu na ujasiri wa Mt. Paulo katika kutangaza Habari Njema.

Ramani ya kufika Kituoni Mt. Paulo Mtume Unga Limited kutoka Friends Corner (inakadiriwa kuwa na umbali wa 1.5km)



2. NJOZI YA KITUO

Kuwa kitovu mathubuti cha Uinjilishaji na Mawasiliano katika Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.

3. UTUME WA KITUO

Kumfanya Yesu Kristo ajulikane, apendwe na afuatwe na watu wote.

4. MALENGO MAKUU NA SHABAHA ZA KITUO

Kituo kina malengo makuu mawili kwa wanafamilia ya Mungu ya Arusha:

a. Kuwa fursa za kupata malezi ya uinjilishaji na uponyaji wa Yesu Kristo kiroho, kiakili na kimwili.

Kutimiza lengo hili kutakuwa na shabaha zifuatazo kwa wanafamilia ya Mungu wa Arusha:

i. Kuwajenga kuwa kweli chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu (*Africa Munus)*.

ii. Kuwapa malezi endelevu waweze kukua na kukomaa katika ufuasi wao na dhamira yao ya kufanana na Kristo katika maisha ya kila siku.

iii. Kujenga na kuimarisha ndoa na familia za Kikristo kulingana na Neno la Mungu na mafundisho ya Kanisa Katoliki.

iv. Kuwajengea uwezo walei wawe viongozi katika Roho ya Injili.

v. Kuwapa fursa ya kupokea Uponyaji wa Kiroho, Kiakili na Kimwili bila hatari ya kupoteza Imani sahihi kwa Mungu na kwa Kanisa.

b. Kupanua uwezo wa Mawasiliano na kufikisha Habari Njema kwa Wanafamilia ya Mungu Jimboni Arusha.

Kutimiza lengo hili kutakuwa na shabaha zifuatazo kwa Wanafamilia ya Mungu wa Arusha:

Jimbo Kuu limeazimia yafuatayo;

I. Kuanzisha Kituo cha Radio cha Jimbo Kuu

II. Kuanzisha Gazeti la Jimbo Kuu.

III. Kuendesha mafunzo ya awali ya Elimu ya Mawasiliano ya Jamii hasa kwa Makatibu wa Parokia, vyama vya Kitume na Mikondo ya Kikatoliki.

IV. Kuendesha semina mbalimbali juu ya mawasiliano mamboleo (athari na faida zake)

V. Kuwezesha uzalishaji wa nyimbo na video zitokanazo na kwaya mbalimbali ndani na nje ya Jimbo letu.

VI. Kujisomea habari za ukweli kwa lengo la kujenga na kuimarisha utu.

5. USIMAMIZI WA KITUO

Kituo kitasimamiwa na Vitengo vya Uinjilishaji na Mawasiliano ya Jamii vilivyo chini ya Idara ya Kichungaji Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.